KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 19, Issue 4

2nd Rabi uth-Thaani 1433

24th Feb, 2012

HUKMU YA ISBAAL KATIKA UISLAMU [Prt 2]

Na: DR. SALEH AS-SALEH

SHUB'HA YA NNE: Baadhi ya watu huchukulia mas'ala ya Isbaal, kuweka Ndevu, na suala zima la mavazi au kudhihirika kwa Muislamu kuwa ni mambo "madogo" au "ya upuuzi". Wao huegemeza maoni yao juu ya ufahamu yakwamba Dini ya Allaah imegawanyika baina ya "maganda" na "kiini". Wanaamini wao yakwamba kudhihirika waziwazi ni katika sehemu ya "maganda." Orodha hii ya mas'ala haya katika Uislamu ni Bid'ah. Kuna ukweli katika msemo usemao yakuwa "Lau kama si kwa maganda, basi kiini kingeliharibika!" Uislamu mzima ni ujumbe uliokamilika. Matendo ya moyo ndiyo yenye kudhihirisha miondoko ya mtu na kuonekana jinsi alivyo. Hii imedhihirika kwenye hadeeth ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema: *"kwa hakika kuna pande la nyama, katika mwili wa mwana-adamu, ambalo iwapo litakuwa ni zuri basi mwili mzima utakuwa ni mzuri, na lau litafisidika basi mwili mzima utafisidika. Kwa hakika hilo pande ni moyo."* [Swaheeh Muslim, V.3, # 3882].

Pia ushahidi unapatikana yakwamba miongoni mwa yenye kudhihirika huwa ni mambo yenyeb kushawishi hali za ndani zenye kufichika. Katika hadeeth iliyopokewa na an-Nu'man Bin Basheer, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Pangeni sawasawa swafu zenu (katika swala) au kwa hakika Allaah atazielekeza nyuso zenu kwenye pande zenye kukhalifiana (yaani; atawateremshia mifarakano miongoni mwenu)."* [Swaheeh Muslim V. 1, hadeeth # 874 na 875]. Katika riwaya nyengine, iliyopokewa na Abu Daawud, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"... au Allaah atazifanya nyoyo zenu zikhitilafiane."* [angalia katika Swaheeh al-Jaami', hadeeth # 1202]. Haya yote yamekusudiwa kuizimua Dini ya Allaah ibakie kwenye ladha ya waume na wake wajichagulie nafsi zao iwapo itawalazimu kushikamana na baadhi ya hukmu zake na sheriya. Kwa hakika sisi tumeamrishwa na Allaah kwa ukamilifu tena kisawasawa, na kwa moyo wote tuingie kwenye Dini ya Uislamu: **"Enyi mlioamini!, ingieni katika hukumu za Uislamu zote, wala msifuate nyayo za Sheitani."** [Al-Baqarah 2:208]. Amesema Ibn Katheer (رحمه الله) katika tafseer yake juu ya aya hii: "Ingieni katika Uislamu na muzitwi'i hukumu zake zote na sheriya zake." Al-Aloosi (رحمه الله) katika tafseer yake amesema kuihusu aya hiyo: "Ingieni kwenye Uislamu kikamilifu na wala msiache chochote kilicho cha ndani mwenu wala nje yenu isipokuwa kiwemo ndani ya Uislamu wenu bila ya kuwacha chumba cha kuingia chochote." [Rooh al-Ma'aani Vol.1]. Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliamrisha, akakataza, akaonya na akaweka mfano wa kuigwa katika suala zima la Isbaal, kuweka Ndevu, kusawazisha swafu kwenye swala, n.k (*na kadhaalika*). Kwahivyo Muislamu na asiyafanye mas'ala haya kuwa ni

'ILMU YENYE MANUFAA

SEMINA YA UKUMBUSHO WA SHEIKH SULEIMAN BIN ALI BIN KHAMIS AL-MAZRU'I

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA
WANAWAALIKA MIHADHARA YA KI-'ILIMU KATIKA MASJID MAZRUI KUANZIA TAREHE 27th FEB - 1st MARCH, 2012 [SIKU NNE]

MAUDHUI NA WAHADHIRI:

1. **YANAYOPASA KUFANYIWA MAITI - ABU BILAL**
2. **RUQYA YA KISHERIYA - USTADH ISMAA'IL**
3. **AT-TARBIYA WAT-TASFIYA - USTADH RAJAB**
4. **SWIFA BAINIFU ZA MTUME - USTADH SHARIFF**

WAKATI WA MIHADHARA

KUANZIA BA'DAL ASR MPAKA ISHAA'
WANAUME WATAKUWA NDANI YA UKUMBI WA MSIKITI NA WANAWAKE WATAKUWA JUU [WANAPOSWALI].

YALIYOMO

ISBAAL [PRT 2]	1 - 4
DARSA ZA 'ILMU	1
HALI YA HATARI SYRIA	4

mepesi kwa sababu kusisitiza/kushikilia juu ya dhambi hata kama ni moja, licha ya udogo wake, huwenda likamsababisha Muislamu kupambana na vitisho vya Allaah: **"Basi walipoendelea na uovu wao, Allaah aliziachilia nyoyo zao zipotoke (kama walivyotaka wenyewe)."** [As-Swaaf 61:5]

Amepokea Sahl Bin Sa'd yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Jitahadharini na madhambi madogo! Ulinganisho wa madhambi madogo ni mfano wa kundi la watu walioshuka chini ya bonde; mmoja (miongoni mwao) akaleta kuni moja, na mwengine akaleta kuni nyengine na mwengine nae (n.k), mpaka wakakusanya kuni zilizowatosha kuutengeza mkate wao. Ni jambo lisilo na shaka yakwamba pindi madhambi madogo yanapomshika mwenye kutenda, humuangamiza mtendaji(mke/ mume).* [imepokewa na Imaam Ahmad na wengineo, angalia katika as-Silsila as -Swaheehah V.1, hadeeth #389].

Amesema 'Ubaadah bin Qurss, "Wewe hufanya baadhi ya mambo yaliyo membamba kuliko unywele kulingana na unavyo ona (yaani; yasiyolaumika katika kuzingatia kwako), lakini katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم), hayo yalizingatiwa kuwa ni makosa makubwa. Msemo huu wa 'Ubaadah bin Qurss uliposimuliwa kwa Muhammad Ibn Sireen, aliuamini na akasema, "Mimi naona yakwamba kuburuta Izaar (nguo yako ya chini) ni miongoni mwa madhambi makubwa kwa sababu ya makemeo makali ya adhabu zilizosimuliwa katika maandiko kuhusiana na mas'ala hayo. Watu huyadhania hayo kuwa ni mojawapo ya madhambi madogo kwa sababu ya ujinga wao mwingi na majivuno ya urongo."

KIPIMO CHA UREFU WA NGUO YA CHINI KINACHORUHUSIWA

Nguo ya chini (*Izaar*) ni lazima iwe juu ya vifundo vya miguu, na imependekezwa zaidi iwe mpaka katikati ya miundi: Amepokea Ibn 'Umar (رضي الله عنه), "Siku moja nilipita mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) nikiwa nimevaa nguo ndefu kupita vifundo vyangu vya miguu. Akaniambia: *'Abdullaah, pandisha juu nguo yako ya chini.'* Nikaipandisha, na akaendelea tena kuniambia, '*Endelea tena kuipandisha juu.'* Nikaendelea tena kuipandisha juu zaidi, na nikawa naendelea kuipandisha juu kidogodogo baada ya hapo, mpaka baadhi ya watu wakaniuliza, 'juu mpaka wapi?' Nae hapo akawajibu, 'Mpaka katikati ya miundi.' [Imepokewa na Muslim, Swaheeh Muslim V.3, hadeeth # 5200].

Akasema Hudhaifa (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliishika misuli ya miundi yangu (au misuli ya miundi yake) kisha akasema, 'Hiki ndicho kipimo cha Izaar. Iwapo hutopendelea (kipimo hicho), ishukishe chini kidogo (yaani; kidogo juu ya ncha za chini za misuli ya miundi). Na iwapo (bado) hutopendelea hapo, basi (ujue yakwamba) ni jambo lisilofaa kwa Izaar kuzidi chini ya vifundo vya miguu.'" [Imepokewa na Ahmad, at-Tirmidhee, an-Nasaa'ee, na wengineo. At-Tirmidhee amesema yakwamba ni hadeeth swaheeh inayokubalika (at-Tirmidhee, kitabu cha mavazi # 1783). Vilevile angalia as-Swaheehah, V.4, # 1765].

Al-'Alaa bin 'Abdur-Rahmaan amepokea yakwamba babake ('Abdur-Rahmaan bin Ya'qoob) amesema: "Nilimuuliza Abu Sa'eed al-Khudhree' (رضي الله عنه) kuhusu vazi la nguo ya chini (Izaar)." Akanijibu: "Wewe umefika kwa mtu mwenye kuyajua vyema mas'ala hayo. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: 'Izaar ya Muislamu inapasa kuwa nusu njia kuelekea chini ya miguu yake– na hatokuwa na makosa iwapo itakuwa ndefu baina ya hapo na vifundo vya miguu, lakini kijacho chini ya vifundo vya miguu ni Motoni. (Katika Siku Ya Malipo), Allaah hatomwangalia yule ambaye atakaeburuta nguo yake ya chini kwa kiburi.'"

Amesema al-Haafidh Ibn Hajar (رحمه الله), "Imekwisha kuamuliwa, kwahivyo, yakwamba kuna hali sampuli mbili kuhusiana na Izaar ya mwana-mume. Hali iliyopendekezwa zaidi ambayo kipimo cha nguo ya chini iteremke hadi katikati ya miundi, na kipimo kinachoruhusiwa ni pale ambapo mpaka wake wa chini ni juu ya vifundo vya miguu." [Fat-hul-Baari V.10, Uk. 259].

TANABAHI! Kuifupisha nguo ya chini mpaka magotini ni Ghuluww (kupindukia mipaka) katika Dini na imeharamishwa.

NI SAMPULI GANI YA NGUO ZILIZOHUSISHWA

CHINI YA SHERIYA ZA *ISBAAL*?

Yanapokuja mas'ala kuhusu *isbaal* kwa wanaume, linalohusika zaidi ni urefu na wala si sampuli ya nguo. Amepokewa 'Abdullaah Ibn 'Umar (رضي الله عنه): "Isbaal ni nguo ya chini, Al-Qameess (kanzu), kilemba. Mtu yoyote atakaeburuta chochote katika mavazi hayo kwa maringo na kiburi, Allaah hatomwangalia katika siku ya Malipo."

Hii yaonyesha yakwamba kuburuta nguo na kuvaa nguo ndefu hayakuwekewa mipaka kwenye Izaar katika sampuli zake zote. Mtu hafai kuzidisha nidhamu za kawaida na desturi zenye kupinga mafundisho ya Uislamu. Kilemba, na vilevile ncha zake hazifai kuwa ndefu zaidi kwa ajili ya kujilinda dhidi ya kiburi na kujitwaza. Baadhi ya vilemba virefu ,vya kisasa huwenda vikahitaji vyombo maalum vya kukisokota! Vilevile kuna kuburuta na kupwaya kwenye mikono mirefu ya nguo hususan katika miji ya Misri na Sudan.

Imaam Ibn al-Qayyim (رحمه الله) amesema: "Mikono mirefu na mipana ya nguo, iliyokaa kama mikoba hayakuwahi kuvaliwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) wala yoyote miongoni mwa Maswahaba zake, na (mitindo yake) ni kinyume cha Sunnah zake. Kuruhusiwa kwake kuna shaka kwa sababu kunahusiana na majivuno ya urongo." Imaam ash-Shawkaani (رحمه الله) aliyaeleza mavazi ya baadhi ya wanavyuoni yakuwa yalikuwa na "mikono mipana kiasi cha kwamba kila mmoja wake unaweza kutengenezwa nguo nzima au shati la mmojawapo wa watoto wao au mmojawapo wa mwana wa yatima." [Naylul Awtwaar V.2, 108].

Ibn Hazm (رحمه الله) amesema katika kumueleza mtu aliye *Musbil*: "Kwa ujumla Isbaal inahusiana na surwale, nguo ya chini, shati, na kila wanachovaa watu." Al-Haafidh Ibn Hajar amemnukuu at-Twabaree akisema: "Katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم), watu wengi walikuwa wakivaa Izaar na Al-'Ardiyah (nguo ya juu iliyo pana, vilemba, joho, n.k). Lakini watu walipoanza kuvaa mashati na aina nyengine za nguo (kama vile majoho n.k), hukmu kama hizo za uharamu zikatumika kwenye kuburuta na kupwaya kwa Izaar katika kuwahukumu wao. Amesema Ibn Battaal: "Hii ni tafsiri nzuri ya ulinganifu. Kwa hiyo, hata kama hakuna maandiko yenye kuhusisha Thawb, makatazo yatahusisha waziwazi zote (yaani; nguo zote zenye kunin'giniya chini ya vifundo vya miguu)." [Fat-hul Baari V.10, Uk.260]

ISBAAL NA SWALA:

Huwenda ikawa umewagundua baadhi ya watu wakikunja au wakisokota nguo zao za chini (haswa surwale) pindi wanapokurubia kuswali. Marejeo yao ni hadeeth iliyopokewa na Abu Daawud ambayo imesemekana

yakwamba: “Allaah haikubali swala ya mtu mwenye kuburuta nguo zake za chini.” Hatahivyo, hadeeth hiyo ni dhaifu. Sheiykh Naasirud Deen al-Albaani amesema: “Isnaad yake ni dhaifu, kwa sababu ya Abu Ja’far, mtu asojulikana kama alivyosema Ibnul-Qattan. Kwahivyo, yoyote aliyeiswahihisha isnaad yake basi alikosea.”

Kwa kuyasema hayo yaliyotangulia, inampasa mtu atahadhari yakwamba mwenye kutia niya ya kuswali ukiwa katika hali ya *isbaal* kutokana na kiburi na majivuno, humsababisha Musbil kupata adhabu kali kutoka kwa Allaah. Amesema Abdullaah Ibn Mas’ud: “Nilimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema, ’Yoyote mwenye kuburuta Izaar yake kwa kiburi na majivuno katika swala, فليس من الله في حل ولأ حرام Allaah hana haja na kumpa hifadha ya msamaha wala ulinzi kwake (kutokamana na Moto au kutokamana na madhambi).’”

Riwaya nyengine imekuja kama *Mawqoof* (yaani; iliyopokewa na Abdullaah Ibn Mas’ud). Inasoma kama ifuatavyo: “Pindi mtu-*Musbil* anaposwali Allaah hana haja na kumpa hifadha ya msamaha wala ulinzi (kutokamana na Moto au kutokamana na madhambi).”

Kwahivyo, *Musbil* na ajuwe yakwamba *isbaal* ni hatia kubwa sana katika wakati anaposwali au wakati mwengine wowote. Vilevile inapasa ijulikane kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliamrisha yakwamba hatufai kufanya *Kaft* katika nguo zetu au nywele zetu wakati tunapokuwa kwenye swala. *Kaft* ni kukunja/kukusanya ncha za nguo pamoja, kufunga fundo (buhusha), kupiga matuta, kuingiza ndani, au kuzifungasha nguo pamoja kabla hujaanza kuswali au wakati unaposwali kwa ajili ya kuzuiya zisitawanyike. Hapa litahusika suala, kwa mfano, la kukusanya pamoja na kuzifunga ncha za nguo (*Thawb*) baina ya miguu wakati mtu anapokurubia kuingia kwenye swala au wakati wa ku-Ruku’ au ku-Sujudu, kuzifunga pamoja ncha za kofia kwenye kichwa au mabega, kuzikunja ncha mbili za chini ya surwale, au ncha mbili za vazi la mikono, n.k. Suala hili lisifahamike vibaya na kuchanganywa na kupandisha nguo kisha ukazikata ncha mbili zilizozidi katika nguo ya chini katikati ya miguu au mpaka kwenye kipimo kinachoweka ncha mbili za chini za *Thawb*, surwale, kikoi, n.k. zikiwa juu ya vifundo vya miguu. Hata kama ncha mbili za chini zitakuwa kwenye sehemu zinazoruhusiwa, hazifai kukunjwa nchani mwake kwa sababu kufanya hivyo ndio kufanya *Kaft*.

Katika hadeeth iliyopokewa na Abdullaah ibn Abbaas (رضي الله عنه), amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *“Mimi nimeamrishwa (na kwahiyo Ummah wake pia) kusujudu juu ya viungo saba: Bapa la Uso (pamoja na ncha ya pua na akaashiriya kwenye pua yake), mikono miwili, magoti mawili na vidole vya miguu miwili, na nikakatazwa nisizifungashe nguo na nywele.”*

KWA MUKHTASAR:

***Isbaal* imeharamishwa kutokana na sababu zifuatazo:**

1. Makemeo ya kuadhibiwa motoni kwa *Musbil*.
2. Maamrisho yaliyo wazi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kupandisha nguo juu ya vifundo vya miguu.
3. Matamshi ya ujumla yaliyo kamilika yenye kuhusiana na *Uharamu* wake.
4. Ukokotezo wa kumfuata Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kujisalimisha na maamrisho yake.
5. Ni *Makheelah* (kujitwaza, Kibri, majivuno n.k)
6. Ni katika kuwaiga wanawake.
7. Ni Israfu.
8. *Musbil* hawezi kujilinda dhidi ya uchafu na najisi.

Sheriya ya mavazi ya wanaume iko chini ya hukmu zifuatazo:

1. Imeharamishwa iwapo zitavuka vifundo vya miguu miwili. *Musbil* anakuwa chini ya makemeo ya kuadhibiwa motoni.
2. *Isbaal* yenyewe ni *Makheelah*.
3. Iwapo *Musbil* atakusudia majivuno na Kiburi, Allaah hatomwangalia katika siku ya Malipo.
4. *Isbaal* haikuwekewa mipaka kwa nguo za chini peke yake. Inahusu pia joho, kilemba, surwale, mikono mirefu ya shati, n.k.
5. Asiyekusudia *Isbaal*, lakini ikawa *Izaar* yake ya chini inanin’giniya na wala sio kwa kupenda kwake si *Musbil.*
6. Kipimo cha urefu cha nguo ya chini chenye kupendekezwa ni mpaka katikati ya miundi miwili, na kipimo chenye kuruhusiwa ni mpaka kwenye vifundo vya miguu.
7. Hazifai kufanana na nguo za *ma-Kuffaar.*
8. Hazifai kuwa ni nguo za majivuno.
9. Hazifai kufanana na nguo za wanawake.
10. Ni lazima ziwe ni nguo zenye kupwaya kiasi cha kwamba sehemu za siri hazifai kudhihirika.
11. Hazifai kuwa na mapicha zilizoharamishwa (viumbe vyenye uhai, wana-adamu na wanyama). Au nguo zilizotokamana na asili isiyokubalika katika misingi ya Uislamu, ikiwemo kuwaiga *ma-Kuffaar*.
12. Imeharamishwa kuvaa Hariri safi (pure silk).
13. Kuvaa pete ya dhahabu, bangili, mkufu, n.k. Yote hayo yamharamishwa.

TANBEEH! Huwenda ikawa umesikiya mijadala mengi kuhusiana na madda ya *Isbaal* katika msikiti ulioko wewe. Natumai yakwamba Allaah (سبحانه وتعالى) amenipa mimi uwezo wa kuyaweka wazi mas’ala haya na kwamba Akuongoze wewe ushikamane na Sunnah na ujiepushe na matamaniwa ya nyoyo.

IMAAM ALIYE DHAALIM, KINYOZI NA MFANYI BIASHARA (MUUZA DUKA)

Suali Muhimu: Iwapo Imaam wa msikiti ananyoa Ndevu zake, anavaa *Isbaal*, au anavuta sigara, jee anafaa kuongoza swala?

Jawabu: Baadhi ya wanavyuoni wana misimamo yakwamba swala nyuma ya Imaam aliye dhaalim haifai kwa sababu ya udhaifu wa Imani yake na Dini. Wengine wana misimamo yakwamba, kwa vile swala yake inakubalika, basi swala ya wenye kuswali nyuma yake vilevile ziko zinakubalika. Rai hiyo ya pili ina uzito mkubwa kutokana na muangaza wa uhakika yakwamba baadhi ya Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) waliswali nyuma ya Waislamu waliotekeleza ukatili mkubwa na wala hawakuziregelea swala zao. Baadhi ya Maswahaba, wakiwemo kina Abdullaah Ibn ’Umar waliswali nyuma ya dhalimu mkubwa Al-Hajjaaj Ibn Yusuf (41-95 Hj / 661-714 C.E) na wala hawakuzigomea swala za Jamaa’ah, kwa sababu swala za jamaa’ah ni miongoni mwa haki muhimu za Muislamu.

Waislamu wenye kufanya mambo ya dhulma hawafai kuchaguliwa kuongoza swala iwapo watapatikana watu wengine wenye kustahiki. Hatahivyo, iwapo kuwageuza wao kutaleta *fitnah* (maafa) miongoni mwa Waislamu katika umoja wao, basi kuswali nyuma ya Imaam aliye dhaalim itafaa.

Suali la 2: Jee, inafaa kwa kinyozi kumnyoa mtu Ndevu kutokana na matakwa ya mwenye kunyolewa? Na vipi kuhusu uuzaji wa vitu vya Haraam?

Jawabu: Ni haraam kwa kinyozi au kwa mtu mwengine yoyote kumnyoa mtu Ndevu, hata kama wameombwa wafanye hivyo. Tendon lao litaangukia chini ya maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى): **"wala msisaidiane katika dhambi na uadui."** [al -Maa'dah 5:2].

Vilevile wenye kuuza vitu vya Haraam vikiwemo tumbaku na sigara. Na wamche Allaah na wawe na wahakikishe yakwamba iwapo watajiepusha na haraam, Allaah atawabarikia katika mapato yao na utajiri wao na awafungulie njia nzuri zilizo halali za mapato yao: **"Na anaemuogopa Allaah, (Allaah) Humtengenezea njia ya kuokoka (katika kila balaa)."** [at-Twalaaq 65:2].

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Enyi watu! Allaah ni Mzuri, na hakubali isipokuwa kilicho kizuri. Na Allaah akawaamrisha waumini kama alivyowaamrisha Mitume kwa kusema:* ***'Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na fanyeni mema, hakika Mimi ni Mjuzi wa (yote) mnayoyatenda.'*** *[al-Mu'minun 23:51]. Na akasema,* ***'Enyi mlioamini, Kuleni vizuri tulivyokuruzukuni, na mumshukuru Allaah, ikiwa mnamuabudu Yeye peke yake.'*** *[al-Baqarah 2:172]. Kisha akamtaja mtu aliyesafiri sana, nywele zake matimutimu na huku amejaa vumbi. Ameinua mikono yake kuyaelekeza Mbinguni (akawa anaomba Du'aa'): 'Ewe Bwana wangu! Ewe Bwana wangu! Haliyakuwa chakula chake ni cha Haraam, kinywaji chake ni Haraam, na nguo zake ni Haraam, na amestawi juu ya Haraam. Sasa maombi yake yatakubaliwaje mtu huyu?."*

Baadhi ya watu huwauzia makafiri yaliyo Haraam wakidhania yakwamba kwa vile wao ni makafiri, basi inaruhusiwa kuwauzia vya halali na vya haraam. Tabia hii, emma inaonyesha ujinga au kufuata mapendeleo ya mafsi kwa upande wa wenye kufanya biashara katika hali hii. Hatahivyo, kiini cha jambo hili ni kwamba watu wanajishughulisha na mambo ya haraam kama njia ya kujitafutia maisha! Inajulikana yakwamba kuna baadhi ya Waislamu wanaouza Nguruwe, tembo, sigara, vilevya n.k. kwa makafiri! Sheitwani huwapambia mambo haya wayaone kuwa ni mazuri! Wanahitaji kutubia kwa Allaah na wamuombe Yeye riziki.

Namuomba Allaah (سبحانه وتعالى), auongoze Ummah wa Waislamu waungane juu ya haki iliyobainishwa na Qur'an na Sunnah iliyo swaheeh, na kama ilivyofuatwa na wale ambao Allaah Alokuwa radhi nao, Maswahaba na wafuasi wao. Namuomba atupe ushindi dhidi ya ushawishi wa mapendelewa yetu ili tuweze kusimama dhidi ya maadui wa Allaah katika kuinua bendera ya Tawheed juu ya ardhi hii.

Namuomba Allaah anisamehe iwapo nimeandika chochote chenye kwenda kinyume na Kitaab cha Allaah na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Namuomba Allaah (سبحانه وتعالى) aibariki juhudi hii kwa kuifikisha kwa wale watakaofaidika nayo mno, na aiongeze kwenye mizani yangu ya amali njema katika Siku Ya Malipo.

HALI YA HATARI SYRIA

NA: Sheikh Mash-hoor (حفظه الله)
Mfasiri: AbdulHaqq ibn Kofi ibn kwesi al-Ashanti.

Suali: Sheikh, mimi nakupenda kwa ajili ya Allaah! Nchini Syria, walinganizi wa upotofu, mtu kama al-Buti anayesababisha watu kuuwawa kutokana na maneno yake, wana nguvu, tafadhali nakuomba uwaunge mkono watu wa Shaam hata kama ni kwa neno moja."

Jawabu: Malaika wamezitandaza mbawa zao juu ya watu wa Shaam na imepokewa katika Sunan ya Abu Daawud kutoka kwa Abdullaah ibn Busr (رضي الله عنه) aliyesema: "Ewe Mjumbe wa Allaah, nichagulie na mimi. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu: *"Juu yako ni Mji wa Shaam, kwani ni utakaso wa Allaah kutoka kwa viumbe vyake ambavyo ndani yake hupatikana viumbe vilivyotakaswa kutokana na watumwa wake. Malaika wamezitandaza mbawa zao juu ya ardhi ya Shaam."* [Hadeeth hii ni swaheeh na imepokewa na Abdullaah ibn Hawaalah (رضي الله عنه) na wala si Abdullaah ibn Busr kama alivyotaja Sheikh Mash-hoor. Imaam al-Albaani amesema kuihusu hadeeth hii katika kuiswahihisha na kuichambua katika kitabu cha Abul-Hassan Ali Ibn Muhammad ar-Rabee' kiitwacho *Fadhaail ush-Shaam wad-Dimishq (Riyaadh KSA: Maktabat ul-Ma'aarif, 1420 AH / 2000 C.E), Uk. 27-31: yakwamba hadeeth inapatikana kutoka kwa: Ibn Asaakir, Taarikh; at-Twabaraani; Sunan Abu Daawud, Musnad Ahmad na al-Haakim. Baadhi ya silsila za hadeeth zimepokewa na al -Irbaad ibn Saariya na Abu Umaamah (رضي الله عنهما)* hadeeth hiyo haina sehemu isemayo kuhusu "Malaika hutandaza mbawa zao juu ya ardhi ya Shaam" kwani hiyo inapatikana katika hadeeth iliyo swaheeh iliyopokewa na Zayd bin Thaabit (رضي الله عنه) na ikapokewa na at-Tirmidhee; at-Twabaraani; Ibn Asaakir, Tareekh Dimishq, Vol.1, Uk. 112-115 na akasema al-Haakim, "Hadeeth ni swaheeh kwa masharti ya mashekhe wawili."

Mwenye kuishi katika mji wa Shaam [Syria, Lebanon, Jordan na Palestine] atapata malipo ya (thawabu za) Muraabit [mkaazi] kwa sharti lazima awe anaihudumikia Dini na awe ni mlinganizi katika Manhaj na tabia njema, na awe ni mwenye kuheshimu mipaka ya Allaah, huyu ni Muraabit katika njia ya Allaah. Yanayotokea Nchini Syria ni kutokana na Hikma za Allaah. Wallaahi, matukio makubwa yanayoendelea hapo ndugu zangu. Kabla ya haya yanayotokea sasa kuzuka, mimi nilikuwa nikitafakari mara kwa mara katika nafsi yangu kuhusu Shaam na Syria. Allaah anapendelea mazuri kwa yatokeayo hivi sasa, Jee Allaah anataka ubora na amri irudi hapo? Mimi natumai yakwamba, yale yanayotokea hivi sasa huko Syria yataleta mazao mazuri kwa ndugu zetu miongoni mwa Ahlus-Sunnah. Kuna vita vilivyodhihiri vya kimadhehebu sasa hivi na watu wenye utawala hapo Shaam (Syria) ni Nusayree Baanitiyyah walio juu ya Baatil. Ibn Taymiyyah amesema kuwahusu wao katika *Mu'jam al-Fataawa:* **"Wao ni hatari sana kwa Uislamu na Waislamu kuliko Mayahudi na Manaswara (wakristo)."**

Wao wana madhara zaidi na kabla ya Baytul-Maqdis kutakaswa kutokamana na wapiganaji wa msalaba, Baatiniyyah wote walikamatwa na kuuwawa. Shaam ni makaburi ya wapiganaji wa msalaba, Shaam ni makaburi ya watu wa mongolia na Shaam ni makaburi ya mafisadi walio waovu na ndani ya Shaam, Sunnah ya Allaah haibadiliki. Kundi la pili la watu wa Dini watatoka katika ardhi ya Shaam, la kwanza litatoka katika ardhi ya Madinah na hii ndiyo Sunnah ya Allaah ambayo aliyotueleza Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwahiyo, ardhi ya Shaam ingalipo juu ya uzuri na linalotarajiwa ni kwamba Allaah ataleta uzuri kwa watu wa Syria na kuwakomboa kutokamana na wasiowaonyesha ulinzi kwao na wasiowajali emma watu wazima wala watoto, vijana wala wakongwe, wake wala waume. Namuomba Allaah ayakomeshe mambo hayo na azitakase ardhi hizi kutokamana na Shirk na Dhulma kwani Yeye Ndiye muweza wa kila kitu.